

## Ndoa za awali na za kulazimishwa

### Early and forced marriage

Swahili/Kiswahili

**Ndoa za awali na za kulazimishwa zipo kinyume na sheria katika majimbo yote ya Australia. Pia ni kinyume na sheria kumpeleka ye yote nchi nyingine kwa ajili ya ndoa ya mapema au ya kulazimishwa.**

Ndoa za awali na za kulazimishwa ni zipo?

Ndoa ya awali ni ambapo mtu anaolewa akiwa chini ya miaka 18. Vilevile inajulikana kama ndoa ya utotoni.

Ndoa za kulazimishwa ni ambapo mtu anashinikizwa, kutishwa au kudanganywa kuolewa kwa:

- > kuwafanya wajihisi kwamba wataleta aibu katika familia yao endapo hawataolewa
- > kufanyiwa vurugu au kutishiwa na watu wanaowapenda
- > kushikilia nyaraka za kusafiria, kama vile pasi ya kusafiria, hadi pale watapokubali kuolewa
- > kuwalaghai na kuwadanganya - kusema kwamba wataenda nje ya nchi kipindi cha likizo au kuishwa pete ya uchumba.

Endapo vitendo vya kitamaduni au kidini viro tofauti na sheria za Australia, daima sheria inatakiwa iwe ya kwanza.

**Sheria ya Australia inasemaje?**

Sheria inasema hivi:

- > watu wenye miaka 18 na kuendelea wana uhuru wa kuchagua kuolewa au kutokuolewa, na nani wa kuolewa nae
- > ye yote chini ya miaka 18 haruhusiwi kuolewa. Ikkidi kuna mazingira ya kipekee, mtoto wa miaka 16 au 17 anaweza kuomba hati ya ruhusa ya kuolewa mahakamani
- > sherehe za ndoa za kimila au kidini na mahusiano yaliyosajiliwa kwa walio chini ya miaka 18 hazipo kisheria.

**Ndoa za mapema na za kulazimishwa mara nyingi hutokea kwa wasichana lakini huweza kuathiri wavulana pia. Wazazi wanaweza kujihisi kushinikizwa na familia au jamii kuendelea na hivi vitendo hata kama wameshakuja Australia. Kama itatokea hii, kumbuka kwamba hizi ndoa ni uharifu na adhabu kubwa itatozwa.**



Government of  
South Australia

Kuwasaidia wazazi kuwa bora Zaidi

## Faida za kutomlazimisha mtu kuolewa katika umri mdogo

Vijana wadogo wasipolazimishwa kuolewa, watakuwa na uwezo mkubwa wa:

- > kumaliza shule
- > kupata kazi nzuri
- > kuwa na ujauzito wenye afya na kujifungua vizuri
- > kuheshimika
- > kuwa mbali na hatari za ukatili, ikiwemo ukatili wa kijinsia.

## Je vipi kuhusu ndoa za kupangwa?

Ndoa za kupangwa zipo kisheria Australia. Ni pale ambapo mtu anakubali kwamba wazazi wake au mtu mwingine amtafutie mtu wa kumuoa/kuolewa. Hata hivyo, wote wanaooana lazima wawe na miaka 18 au zaidi na wawe huru kuikubali ndoa.

## Kupata msaada

Pata msaada moja kwa moja kama unamfahamu yeyote yupo katika hatari ya kuingia katika ndoa za awali na za kulazimishwa au anataka kupelekwa nchi nyingine kwa ajili ya kuolewa. Unaweza:

- > kuwasillana na watoa huduma. Ni wasiri. Unaweza kuomba mkalimani
- > kuwapigia Polisi
- > kupiga simu Kitengo cha Taarifa kuhusu Watoto Wanaonyanyaswa
- > kuzungumza na wafanyakazi shulenii.

**Ndoa za awali na za kulazimishwa hudhuru afya na maisha mazuri ya vijana wadogo na zinakiuka haki za binadamu.**

## Huduma

### SA Polisi (SA Police)

000 ikiwa mtu yuko katika hatari sasa  
13 14 44 ikiwa kuna hatari, lakini siyo sasa hivi

### Polisi ya Shirikisho la Australia (Australian Federal Police (AFP))

13 12 37 AFP imefundishwa hasa ili kuwasaidia watu katika hatari ya ndoa ya kulazimishwa  
[www.afp.gov.au/what-we-do/crime-types/human-trafficking](http://www.afp.gov.au/what-we-do/crime-types/human-trafficking)

### Simu kwa ajili ya kutoa Taarifa kuhusu Unyanyasaji wa Watoto (Child Abuse Report Line)

13 14 78 muda wowote mchana au usiku  
Kama wewe au yeyote anajua msichana aliye hatarini  
[www.childprotection.sa.gov.au/reporting-child-abuse](http://www.childprotection.sa.gov.au/reporting-child-abuse)

### Simu kuhusu Vurugu za Majumbani (Domestic Violence Crisis Line)

1800 800 098 muda wowote mchana au usiku  
Msaada kuhusu vurugu, malazi ya dharura na uhamisho  
<http://womensafetyservices.com.au>

### Tume ya Kutoa Huduma za Kisheria SA (Legal Services Commission of SA)

Simu kwa ushauri 1300 366 424, saa 3 asubuhi-saa 10.30 jioni, Jumatatu hadi Ijumaa  
Ushauri wa bure wa kisheria [www.lsc.sa.gov.au](http://www.lsc.sa.gov.au)

### Idara ya Mambo ya Nje na Biashara (Department of Foreign Affairs and Trade)

1300 555 135 muda wowote mchana au usiku ikiwa wewe uko Australia na unahitaji msaada +61 2 6261 3305  
SMS +61 421 269 080 kama uko nje ya nchi <http://dfat.gov.au>

### Kuzuia Utumwa Australia (Anti-Slavery Australia)

02 9514 8115, saa 3 asubuhi-saa 11 jioni, Jumatatu hadi Ijumaa au barua pepe [antislavery@uts.edu.au](mailto:antislavery@uts.edu.au)  
Ushauri wa kisheria na uhamiaji kuhusu utumwa, biashara na utaratibu kama wa utumwa [www.antislavery.org.au](http://www.antislavery.org.au)

### My Blue Sky

Maelezo juu ya ndoa ya lazima na njia za kutoa ushauri wa kisheria kwa bure [www.mybluesky.org.au](http://www.mybluesky.org.au)

### Msalaba Mwekundu Australia (Australian Red Cross)

8100 4666, saa 3 asubuhi-saa 11 jioni, Jumatatu hadi Ijumaa au 1800 986 401 baada ya saa za kazi au barua pepe [National\\_STPP@redcross.org.au](mailto:National_STPP@redcross.org.au)  
Ikiwa ungependa msaada wa kuwasillana na Polisi ya Shirikisho la Australia [www.redcross.org.au/get-help/help-for-migrants-in-transition/trafficked-people](http://www.redcross.org.au/get-help/help-for-migrants-in-transition/trafficked-people)

### Huduma ya Ukalimani na Tafsiri (Translating and Interpreting Service (TIS National))

13 14 50 kwa wakalimani wa bure wa kwenye simu muda wowote mchana au usiku [www.tisnational.gov.au](http://www.tisnational.gov.au)

Mwongozo huu rahisi wa Mzazi ni mmoja kati ya 9 iliyoundwa na Parenting SA kwa ajili ya familia kutoka kwenye jumuiya mpya zenye tamaduni mbalimbali na zinazoendelea kujitekeza Australia ya Kusini. Tungependa kushukuru mashirika mengi pamoja na familia ambazo zimechangia bure maarifa na utaalam kwenye Miongozo, hasa familia na wafanyakazi ambao picha zao zinaonekana ndani yake.

Parenting SA inashirkiana na Idara ya Elimu na Mtandao wa Afya wa Wanawake na Watoto.

**Simu (08) 8303 1660**  
[www.parenting.sa.gov.au](http://www.parenting.sa.gov.au)

**Mwongozo Rahisi wa Wazazi unatolewa bure Australia ya Kusini**

**Muhimu:** Taarifa hii haikusudii kuchukua nafasi ya ushauri kutoka kwa mtaalamu.

© Serikali ya Australia ya Kusini Toleo la kwanza 01/2019.



Government  
of South Australia